OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI KIFANYA
S.L.P 414
NJOMBE
TAR _Des.2020
Simu: HOS **0755644663,**
S/M **0754548022**

Kumb:KIF/NTC/SE/JOIN. F I/2021

Jina la Mwanafunzi _____

Shule ya Msingi _____

NJOMBE.

YAH**: MAAGIZOYA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIFANYA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**

1. UTANGULIZI

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2020**. Shule ya Sekondari Kifanya, ipo umbali wa Km 0.4 Kaskazini, Magharibi mwa mji mdogo wa Kifanya, kutoka Njombe Mjini kuna umbali wa Km 50 kupitia barabara ya kwenda Songea. Usafiri wa Noah unapatikana katika Stendi kuu ya Mji Mwema. Nauli ni shilingi 3000/= tu.
Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **06/01/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **13/01/2020**

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- **SARE YA SHULE**

(i) SARE YA DARASANI

WAVULANA

a) Suruali mbili zenye linda moja ya rangi ya daki bluu(dark blue) naya pili rangi ya damu ya mzee (Sio za kubana chini) na shati mbili za mikono mifupi kwa ajili ya darasani
b) Suruali mbili za rangi ya zambarau na fulana mbili za rangi ya bluu, hizi ni nguo za kazi za nje.
c) Sweta rangi ya bluu, vesti mbili nyeupe, soksi nyeusi pea mbili au zaidi na viatu vya rangi nyeusi (visiwe vya mchongo) viwe vya kufunga na kamba na nguo za ndani za kutosha. (chupi 05 boxer)
d) Tracki suti ya rangi ya dark bluu,(**isiwe bluu wala nyeusi**) yenye michirizi nyeupe

WASICHANA

a) Gauni mbili, moja ya rangi ya daki bluu (dark blue) na ya pili damu yamzee inayofika kwenye magoti za kukata mikono, suruali moja ya daki bluu(dark blue) na ya pili damu ya mzee na mashati mawili ya **mikono mifupi**
b) Gauni mbili za rangi ya zambarau ndefu za kuvuka magotini, mikono mirefu, zenye ukosi hazitavaliwa na suruali yenye malinda boksi
c) Sweta rangi ya bluu, vitopu vinne(04)au zaidi vya rangi nyeupe, soksi nyeusi pea mbili, viatu vya rangi nyeusi viwe vya kufunga na kamba pia nguo za ndani za kutosha (CHUPI 06NA TAITI 03 au zaidi)

(ii) Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule

(iii) SARE ZA MICHEZO

a) WAVULANA
Kwa shule hii ni bukta mbili na Tshirt mbili za rangi ya bluu, track suti moja rangi ya daki bluu(**isiwe bluu wala nyeusi**), raba za michezo na soksi ndefu ya rangi ya bluu.

b) WASICHANA
Trakisuti rangi ya daki bluu**(isiwe bluu wala nyeusi),** viatu vya michezo pea mbili, soksi ndefu rangi ya njano na Tshirt rangi ya bluu.

NB: • Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani hapa KIFANYA SEKONDARI. Nikosa kwa mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani hapa Shuleni,hatuakali za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi atakayekiuka utaratibu huo isipokuwa kwa mwanafunzi wa kike anaruhusiwa kutumia kanga au kitenge anapo oga.

• Kila mzazi /mlezi ahakikishe kuwa vifaa vyote vya mtoto wakovimewekewa alama/jina linalosomeka na kuonekana ili kuepuka migongano isiyoyalazima kwa wanafunzi wengine wenye vifaa vinavyofanana.

iv) **Daftari** 12 au zaidi (3 quire) Kalamu, mfuto, biki za rangi ya bluu au nyeusi za kutosha, jalada (faili) aina ya boksi la kutunzia karatasi za mitihani na majaribio, flati faili la kuhifadhia taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi ofisini (liwe la plastiki la bluu) na mkebe wa hesabu.

3. <u>MICHANGO</u>

i) **Chakula** cha wanafunzi Mahindi kilo 240, Maharage (soya, kaki, magereza kilo 60, mchele kilo 20 vyakula hivi vitatumika mwaka mzima kwa mwanafunzi anayekaa hosteli, lakini kwa Yule atakayekaa nyumbani atatakiwa kulipa: Mahindi kilo 120 na maharage kilo 30 (soya, kaki, magereza) kwa mwaka mzima. Vyakula hivi mzazi/mlezi anatakiwa kulipa kwa awamu mbili, nusu ya mchango muhula wa kwanza mwezi Januarina nusu ya pili muhula wa pili mwezi Julai, kwa kila mwaka wa masomo.

ii) **Fedha**Utatakiwa kuchangia fedha Tshs 136,000/= kwa mwaka, kwa ajili ya kusaga, **kununua** kuni na usafirishaji, chumvi, mafuta, sukari, nyama, mboga za majani na malipo ya wapishi na mhudumu. Fedha hii unaweza kulipa yote au kwa awamu mbili kulingana na mihula ya shule (Shule inapofungua)

Michangoyote ya Fedha ilipwe kwenye BANK ya NMB au SACCOS YA KIFANYA (Wakala wa NMB) kwenye akaunti namba 60610003605. Jina la akaunti KIFANYA SEKONDARI (Akaunti inayoishia …….02 ambayo ilikuwa inatumika awali haipo kwenye mfumo wa malipo ya serikali kwa sasa). Baada ya malipo stakabadhi (Bps) zote ziwasilishwe shuleni.

TANBIHI: FEDHA TASLIMU HAZIPOKELEWI SHULENI

4. VIFAA: Mahitaji mengine ya kibinadamu (Zingatia sana maelekezo ya rangi ya vifaa vya kila sehemu)

Vyombo vya kutumia kulia chakula (Kontena na kikombe) hutumika kwa mwaka mmoja. Kuhusu rangi kila Darasa lina rangi yake na HAIBADILIKI hivyo kila mzazi/mlezi utatakiwa kumnunulia mtoto wako kifaa kipya cha rangi ya darasa analoingia mwanao (kila chombo kiandikwe jina lake)(i) kidato cha I.....rangi ya KIJANI

(ii) kidato cha II.....rangi NYEKUNDU

(iii) kidato cha III.....rangi ya BLUU

(iv) kidato cha IV.....rangi ya PINKI

NB: Uamuzi huu umewekwa ili kuondoa tabia ya wanafunzi wa madarasa mengine kuchukua vyombo vya madarasa yasiyo yao.

a) Sanduku imara la bati au mbao na kufuli kwa ajili ya kuhifadhia vitu vya mwanafunzi
b) **- Ndoo moja ya lita 10 rangi ya kijani kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi na ndoo ya lita 20 (Amboni) rangi ya bluu kwa wasichana (kwa matumizi ya** kuchotea maji ya jikoni)
   - Ndoo moja ya lita 10 rangi ya kijanikwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi na jembe jipya moja lenye mpini kwa wavulana.
c) Godoro la futi mbili na nusu (ft 2.5 x 6) aina (Dodoma) **unene** ni Inch 4**(Kwandani liandikwe jina la mwanafunzi**) kinyume na vipimo hivyo halitapokelewa
d) Blanket moja zito na shukambili za rangi ya kijani folonya ya rangi ya kijani
e) Ufagio wa chelewa mmoja na kila muhula
f) **Wavulana** waje na taulo,bukta 02, sabuni za kuogea na kufulia za kutosha
g) Wasichana waje na taulo, kanga au kitenge doti mbili, sabuni za kuogea na kufulia za kutosha (**vipodozihaviruhusiwi kabisa hapa Shuleni)**
h) **Wavulana** au wasichana waje na brashi za kufulia raba na za kung'arisha viatu na dawa yaviatu vyeusi vya darasani.

5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

(i) Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na**Wizara yenye dhamana ya masuala ya Elimu** nchini na **Ofisi ya Rais – TAMISEMI** zenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Evening Preparation) ni lazima
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za Umma.

(ii) Makosa yafuatayo yanasababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule

a) **Wizi**
b) **Uasherati na ushoga**
c) **Ubakaji**
d) **Ulevi na utumiaji wa dawa za kulevya kama bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k**
e) **Kupiga au kupigana**
f) **Kuharibu kwa maksudi mali za shule**
g) **Kudharau bendera ya Taifa**
h) **Kupata mimba/Kusababisha mimba, Kuoa au kuolewa**
i) **Kutoa mimba**
j) **Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.**
k) **Kukataa adhabu kwa maksudi**
l) **Kuwa na simu ya mkononi**
m) **Utoro Sugu**

6. **<u>MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI</u>**.

(i) **Medical Examination Form** ambayo itajawza na**MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia fupi ya mwanafunzi na mkataba kwa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
(iii) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
(iv) Mchango wa Bima ya afya kwa kila mwanafunzi Tshs 5000/= kwa mwaka

7. Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Nakutakia maandalizi mema ya kuja kuripoti shulen kwa wakati ukiwa umevaa sare ya darasani, tayari kukaguliwa na kwenda bwenini kuweka vifaa, nawe kuingia darasani mara moja.

KARIBUNI KIFANYA SEKONDARI

“HAPA NI KUSOMA TU”

_____

HILUKA E.M

MKUU WA SHULE